# READY

RESILIENT & EMPOWERED ADOLESCENTS & YOUNG PEOPLE

#WeAreREADY

JARIDA LA MRADI WA READY #13 | FEBRUARI 2024



UTAYARI wa kuunganika na kujifunza.

Watetezi wa Vijana wahitimisha Mkutano wa Kilele wa Mradi wa READY uliofanyika Harare, Zimbabwe. © Y+ Global/ Hukastone Studio 2023



Pedro, Angola

**Karibu kwenye toleo la 13 Jarida la READY! Toleo hili linazingatia suala la ushirikishwaji na mafunzo.**

READY inatoa majibu ya changamoto za kijamii zinazowaathiri vijana balehe na wadogo katika utofauti wao wote. Watu wanahitaji kuhamasishwa na kuhusushwa kihisia ili kuchochea harakati na mikakati kwa ajili ya mabadiliko katika jamii.

Na kila kiongozi anapaswa kujifunza mbinu za mabadiliko ili abakie kuwa na umuhimu katika ulimwengu unaoendelea kubadilika kila mara. Kwa hiyo, mwezi Desemba, 2023, tuliandaa mkakati mpya kwa jina la **READY to Evolve**, ili kuongeza ushiriki wa vijana na kuunganisha nguvu zao kwa lengo la kuongeza ushirikiano wa kikanda na wa ndani. Ushiriki wangu kwenye mkutano wa READY uliofanyika mwezi Desemba uliopita nikiwa kama kiongozi uliweka alama kwenye maisha yangu pamoja na ushindi ambao vijana wameupata tangu harakati zilipoanza katika kuwahamasisha ili kulinda haki zao na kutimiza majukumu yao.

READY inasimamia taarifa, mafunzo, kuwasikiliza vijana wadogo, kuwajengea uwezo viongozi vijana na kushirikishana mikakati yenye tija ili kufikia matokeo. Kwangu mimi, kama kijana na kiongozi kwenye jamii yangu, mwaka 2023 ulikuwa ni mwaka wa mafunzo endelevu. Kwa upande wa harakati, maadili ni jambo la msingi. Uongozi sio tu jambo la cheo: ni kuwajibika ili kuwatetea wale wasioweza kujisemea, kila wakati kutumia ubunifu kama njia bora zaidi ya kuthamini na kutatua matatizo kwenye ulimwengu wa kihalisia.

*Pedro Kakoka*

*Pedro J. Almeida Kakoka*
KIONGOZI, READY, ANGOLA

## ICASA 2023 yaunganisha vijana katika kutatua changamoto za usawa na kutokomeza UKIMWI, kupitia mkutano wa READY



Vijana wakiwa kwenye picha ya pamoja kwenye mkutano wa READY uliofanyika Harare, Zimbabwe © Y+ Global/Hukastone Studio 2023

NA, TUMIE KOMANYANE, KIONGOZI WA PROGRAMU (VIJANA RIKA BALEHE NA WADOGO)SHIRIKA LA FRONTLINE AIDS NA TINASHE RUFURWADZO, MENEJA WA MAWASILIANO NA USHIRIKISHWAJI WA KIDIGITALI, MTANDAO WA VIJANA WANAOISHI NA MAAMBUKIZI YA VVU DUNIANI (GNP+)

Katika onyesho la nguvu la ahadi kwa vijana ulimwenguni katika harakati za kujenga na kuimarisha vijana, Mkutano wa kilele wa READY uling'ara Zaidi katika mkutano wa kimataifa wa ICASA 2023 huko Harare, Zimbabwe. Tulizindua mkakati wetu, tulioupa jina la READY to Evolve, tukionyesha ahadi yetu katika kuongoza mwelekeo wa uongozi wa vijana katika VVU na Haki ya Afya ya Uzazi na Ujinsia (SRHR) Mashariki na Kusini mwa Afrika. Kwa wiki nzima, mkutano wa READY uliibuka kama kichocheo cha ushiriki na ujenzi wa vijana

Dk. Margret Verwijk, Balozi wa Ufalme wa Uholanzi anayewakilisha nchi za Zimbabwe, Zambia na Malawi alisema kwamba "kwa kuwashirikisha vijana, kwa kuwaweka katika mstari wa mbele kwenye masuala yanayoathiri maisha yao, miradi kama hii inaweza kufikia maono yake ya muda mrefu kwa kutumia mbinu muafaka, zenye malengo mahsusi na yenye kutoa matokeo tarajiwa".

Daktari Verwijk alisisitiza ubunifu, jitihada na matumaini ambayo vijana hutumia akikazia kwenye jitihada shirikishi zinazotakiwa ili kutokomeza UKIMWI na kuboresha haki za afya ya uzazi. Vyombo vya habari vilinasa mijadala kwa kina katika mkutano wa READY. Vipindi vilivyo sheheni washiriki, vikiongozwa na vijana na Tumie Komanyane, viliangazia mpango mkakati na majadiliano yenye kuchochea fikra huku yakikuza sauti yenye ushawishi ya mradi wa READY katika kutoa mwelekeo wa ajenda za mkutano.

Mapendekezo ya msingi yalisisitiza umuhimu wa kuwashirikisha vijana wakati wa kufikiwa kwa maamuzi. Washiriki pia walisisitiza haja ya kuwepo kwa mfuko maalumu wa kusaidia programu za vijana. Mada ya ushauri ilijitokeza mara nyingi ikichochea utekelezaji wa ahadi ya kukiunga mkono kizazi kijacho .

Matokeo ya harakati za READY zilisambaa hata nje ya kumbi za mkutano. Kwa kutetea sauti za vijana mkutano wa READY unaonesha kwamba njia ya jumuishi, ya majibu yenye ufanisi kwa VVU iko mikononi mwa vijana kwa kuzingatia utofauti wao wote. Na tubebe mwenge unaotoa mwanga wenye ujumbe unaosema "hakuna kitu chochote kwa ajili yetu, bila ushiriki wetu", tukuze ushiriki wenye maadili, tuwezeshwe na kupewa ushauri wenye tija ili kuandaa maisha ya baadaye ambapo vijana ndiyo wanaendelea kuongoza.

## UCHAMBUZI WA WASHIRIKA WA KIKANDA

### Young Africa

Na CONCILIA MUTAMI, MSAIDIZI WA PROGRAMU, MAWASILIANO, SHIRIKA LA YOUNG AFRICA

Zaidi ya vijana 500 wakisaidiwa na READY+ katika nchi za Msumbiji na Zimbabwe, wamejiandikisha kwa mafunzo ya ufundi stadi waliochangua wenyewe kupitia mradi wa Skills2 Live. Lauri*, mwenye miaka 20, kutoka Beira, Msumbiji, ni mmojawapo wa wanafunzi wengi waliopendekezwa na READY+ kuhudhuria mafunzo kwenye shirika la Young Africa. Alisema mwaka 2021, "kupitia mradi wa Skills2Live, nilipata ufadhili kwa ajili ya kuhudhuria kozi ya mafunzo ya ufundi. Nilisomea ufundi wa bomba. Ninatoa shukrani kwa harakati za READY na mradi wa Skills2Live. Sasa ninaweza kuchangia gharama za fedha zinazohitajika nyumbani kwangu. Ingependeza kama mradi wa Skills2Live ungeendelea ili kuwasaidia vijana wengine wadogo kama mimi" Kwa kupitia ushirikiano kati ya shirika la READY+ na Young Africa, mradi wa Skills2Live umewawezesha vijana wenye maambukizi ya VVU kwa:

- Kuwa na uwezo ulioboreshwa wa kutafuta msaada kutoka kwa watu wengine. Vijana wanajua umuhimu wa msaada unaoyokidhi mahitaji yao, hatari na madhara ya misaada mbalimbali na wana uwezo wa kukuza upatikanaji wa huduma mahsusi.
- Ongezeko la maarifa, uwezo, kujithamini na kujiamini ili kufanya mabadiliko kwenye maisha yao. Kwa kupata mafunzo ya ufundi stadi, fursa za vijana za kuajiriwa au kuanzisha biashara zao ndogondogo zinaboreshwa. Pia wanajisikia kuwa salama kujadili matatizo yao ya kiafya na wanasaidiwa kupata huduma za afya ya uzazi na ujinsia kwenye vituo vya afya.
- Kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi ulioboreshwa ndani ya kaya, jamii na kwenye uchumi wa ndani, ukisambaa kwenye maeneo ambayo kijadi yanajulikana kuwa ya mfumo dume. Hii inajumuisha vijana kufanya maamuzi kuhusu afya yao ya uzazi na ujinsia.

Ushirikiano huu kati ya READY+ na mradi wa Skills2Live unadhihirisha uhusiano kati ya uwezeshaji kiuchumi na afya ya uzazi na ujinsia kupitia afua za VVU. Ni Dhahiri kwamba vijana wadogo wanahitaji kuwezeshwa ili waweze kuamua kwa uhuru mambo yanayohusu haki zao za afya ya uzazi na ujinsia.

**Majina sio halisi.*

Endelea kutazama eneo hili kadri tunavyoendelea kukusanya simulizi kutoka kwa shirika la READY+ na washirika wake wa kikanda wanaofadhiliwa na Ubalozi wa Uholanzi jijini Maputo.

## Vijana katika mkutano wa ICASA 2023

22nd ICASA INTERNATIONAL CONFERENCE ON AIDS AND STIs IN AFRICA 4-9 December 2023 Rainbow Towers, Harare, Zimbabwe



Ibrahim Kalimbaga, 25, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***Jukumu lako kwenye mkutano lilikuwa ni lipi?***
Niliwakilisha vijana wenzangu watoa huduma kwa kundi rika katika jamii (CATS), kama mwanachama wa mtandao wa vijana wanaoishia na VVU Tanzania (NYP+)

***Ulijifunza nini?***
Kuhudhuria ICASA 2023, ulikua ni uzoefu wa kipekee lililonipatia manufaa jinsi ya kuboresha upatikanaji wa huduma za VVu na afya ya uzazi na ujinsia na mikakati ya uchehemuzi kimataifa.

***Utayatumiaje maarifa haya?***
Hatua ya kwanza ni kushirikishana maarifa haya na wenzangu ili kuboresha kazi na kutumia ubunifu kwa ajili ya kuboresha maisha ya baadaye.



Ercilia Benedito Saide, 21, Msumbiji.

***Jukumu lako kwenye mkutano lilikuwa ni lipi?***
Nikiwa kama kiongozi kwenye mradi wa Y+Global, niliwakilisha vijana. Jukumu langu lilikuwa ni kuongeza maarifa na ujuzi katika nyanja za uchechemuzi na uongozi ili kwenda kuvitumia nitakaporudi nchini mwangu.

***Ulijifunza nini?***
Nilijifunza kwamba ili niwe kiongozi mzuri ni lazima tufanye kazi kwa ushirikiano kwa lengo la kufikia matokeo ya kuridhisha. Pia nilijifunza jinsi tunavyoweza kuendelea katika njia iliyo bora kwa kuwa bado tunakabiliana na unyanyapaa na ubaguzi.

***Utayatumiaje maarifa haya?***
Kwa kupitia mikutano tunayoandaa kwa kuwashirikisha vijana kwenye vituo vya afya na kwenye jamii na kwa kupashana habari kwa njia ya mtandao na podikasti.

# Kongamano la Mradi wa MenEngage Africa kuhusu Haki na Afya ya Uzazi na ujinsia

NA,TAWANDA CHIBONORE, MTAALAMU WA MIUNDO NA PICHA ZA MITANDAONI, MTANDAO WA KIMATAIFA WA VIJANA WANAIOSHI NA VVU (Y+ GLOBAL)

Hivi karibuni nilihudhuria Kongamano lililoandaliwa na mradi wa MenEngage Africa kuhusu Haki na Afya ya Uzazi na Ujinsia kwa wote: Kujenga Maisha bora yajayo kwa vijana wa Afrika. Mada hii ilishabihiana kabisa na malengo ya harakati za mradi wa READY, kwa kuwa jitihada zote zinashirikisha maono ya kuwawezesha vijana kusimamia afya zao kuhusu masuala ya afya ya uzazi ya ujinsia ambayo hatimaye hutoa mwelekeo wa maisha yao ya baadaye. Kipengele muhimu kilichoibuka wakati wa kongamano kilikuwa ni haja ya kuwashirikisha wanaume na wavulana kwenye majadiliano kuhusu Haki na afya ya uzazi na ujinsia.

Kwa kuwashirikisha wanaume na wavulana, kanuni zenye madhara zinaweza kukabiliwa na pia vikwazo vya huduma za kina kuhusu haki na afya ya uzazi na ujinsia kuondolewa. Kongamano lilisisitiza muingiliano wa kimapenzi: jinsi haki ya afya ya uzazi na ujinsia zinavyoingiliana na harakati nyingine za haki za kijamii kama vile haki na usawa wa kijisia wa kundi la watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja. Tulijadili haja ya kutambua na kukabiliana na vikwazo mahsusi wanavyokumbana navyo watu wanaotoka kwenye jamii zinazobaguliwa.

Harakati za mradi wa READY zinashirikishana mtazamo huu na kujitahidi kutoa uwanja salama kwa vijana wote bila kujali mazingira waliyotoka. Umuhimu wa kuwashirikisha vijana kwenye vikao vya maamuzi ulikuwa ni mada iliyojirudiarudia kila wakati kwenye kongamano hili. Vilevile mradi wa READY unazingatia kulea uongozi wa vijana, kusaidia kupaza sauti zao na kuijumuisha mitazamo yao kwenye sera na programu.

Kongamano liliimarisha mahusiano na harakati za mradi wa READY. Kwa kukubali umuhimu wa kuwashirikisha wanaume na wavulana , kuboresha muingiliano wa kimapenzi na kuwezesha vijana katika jitihada zao za kupata huduma za haki na afya ya uzazi na ujinsia, mikakati hii miwili inaweza kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufikiwa kwa mabadiliko chanya na kulea jamii zenye afya bora zaidi. Ushirikiano huu utakuza athari na kusukuma maendeleo kuelekea dunia ambapo kila kijana anakuwa na uchu wa kustawi.

# Matokeo ya kampeni ya mradi wa READY to Thrive kwenye mitandao ya kijamii



Wahamasishaji wa mtandao wa Kijamii © Miguel Osorio 2023

NA, MIGUEL OSORIO, MRATIBU WA PROGRAMU: "READY FOR AN AIDS FREE FUTURE" NCHINI MSUMBIJI.

Chini ya programu ya READY for an AIDS free Future (Utayari wa Maisha ya baadaye yasiyo na UKIMWI), tulibuni kampeni ya Ready To Thrive ili kuwafikia vijana wadogo kupitia mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Instagram na TikTok. Kampeni hii ilisambaza Jumbe kuhusu afya ya ngono, zikizingatia kinga dhidi ya maambukizi ya VVU, upimaji , tiba na misaada kwa watu wanaoishi na VVU. Timu ya wataaamu wa ukaguzi ilihakikisha matumizi ya lugha yenye staha, walichunguza maudhui na kukagua mawasilisho kabla ya kuyachapisha.

Wahamasishaji wawili wanaojulikana – Fidamae 2x na Salesio Do Panico – walisaidia kubuni maudhui yenye mvuto na yaliyo sahihi. Kwa kufanya kazi kwa karibu na timu ya Utaalamu ya VVU ya Mradi wa Utayari wa Maisha Ya baadaye yasiyo na UKIMWI ( kwa kiingereza Ready For an AIDS Free Future -R4AFF's ) walibuni picha fupi , yenye nguvu na mafundisho inayotoa pendekezo la suluhu ya tabia za hatari, kuondoa simulizi na kuhimiza ngono salama. Muunganiko huu wa ucheshi na taarifa za afya ulithibitisha ufanisi wa hali ya juu katika kuwashirikisha vijana.


Mafunzo yaliyofunzwa ni pamoja na kuhakikisha muktadha mahsusi , taarifa fupifupi na ubora wa lugha. Kujumuisha upimaji wa VVU na kushirikiana na wataalamu wa huduma za afya kutasaidia kuimarisha matokeo ya kampeni zijazo pia. Mradi wa Ready To thrive ulifanikiwa katika kuelimisha vijana wadogo, kuongeza ufahamu na kuondoa uwepo wa VVU. Fidamae 2x na Salesio Do Panico walipanua uwanja wa eneo la kampeni na ufanisi, kwa mikanda miwili ya picha iliyotengenezwa na Salesio ikipata watazamaji karibu nusu milioni. Kijana mmoja mdogo alitoa maoni yake:

> "Nimependa maudhui. Ukweli hii inaweza kusaidia watu wengi ili waelewe kwamba kuishi na VVU sio mwisho wa dunia.

Kwa kutumia mikakati yenye ubunifu kuwashirikisha vijana kwenye makundi yao mafanikio ya kampeni yanaonesha uwezo mkubwa wa mitandao ya kijamii katika kukabiliana na masuala nyeti ya afya miongoni mwa vijana. Mradi wa Ready To thrive ulikuza utamaduni wa ongezeko la ufahamu na uwajibikaji, jambo ambalo ni mchango mkubwa wenye ufanisi katika kupunguza unyanyapaa unaoambatana na VVU. Picha hizi zinabakia kuwa kwenye kurasa za wahamasishaji hawa na zitaendelea kuwaelimisha vijana.

- Facebook: Fidamãe 2x | Instagram: @Fidamãe 2x
- Facebook: Salésio Do Pânico
- Instagram: @Salésio Do Pânico

# Vijana katika mkutano wa ICASA 2023



Lusungu Harawa, 26, Malawi

***Jukumu lako kwenye mkutano lilikuwa ni lipi?***
Niliwajibika kuandaa malengo ya Kongamano la READY tukishirikiana na Tumie aliyehudumu kwenye shirika la Frontline AIDS. Pia niliwasilisha mada kwenye kikao maalumu cha ngazi ya juu cha mkutano huu kilichohusu vijana.

***Ulijifunza nini?***
Ushirikishwaji wa jamii ni muhimu sana katika kukabiliana na janga la VVU na maambukizi yanayotokana na vitendo vya ngono barani Afrika. Kuwajenga na kuwawezesha vijana kuongoza ni muhimu.

***Utayatumiaje maarifa haya?***
Tunahitaji sauti imara za vijana ili kushirikiana na serikali na asasi zisizo za serikali nchini mwangu kwa lengo la kutokomeza UKIMWI kwa kutumia rasilimali na utaalamu ili kufikiwa kwa matokeo yaliyoratibiwa vizuri.

# Kumbukumbu zangu kuhusiana na Mradi wa READY+

NA, DAKTARI FATIMA ALY, AFISA WA SERA ZA HAKI YA AFYA UZAZI NA UJINSIA, NA VVU / UKIMWI, UBALOZI WA UFALME WA UHOLANZI, MAPUTO.

Umekuwa ni upendeleo mkubwa kuwa sehemu ya programu ya Haki na Afya ya Uzazi na Ujinsia na VVU/UKIMWI ya Kanda ya Afrika ya Kusini, hasa mradi wa READY+. Tangu nilipojiunga na ubalozi wa Uholanzi jijini Maputo mwaka 2014 nimeshuhudia mabadiliko chanya na matokeo mazuri pamoja na yale yaliyofikiwa na mradi wa READY+

Mradi wa READY+ unayafikia moja ya makundi yanayoishi katika mazingira hatarishi zaidi katika ukanda huu: vijana walioathirika na VVU. Mradi huu unawawezesha kuwa na maisha bora ikiwa ni pamoja na huduma ya Haki na Afya ya Uzazi na Ujinsia na athari za VVU na ufahamu, uharaka na uhuru wa kuamua kuhusu maisha yao.Ninaamini kwamba mradi wa READY+ unausadia ukanda huu kufikia malengo yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030 kwenye mpango wa malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Nikiwa kwenye ziara za kutembelea miradi katika nchi mbalimbali ambako miradi ya READY+ inaendelea nimeshuhudia ushirikishwaji na kazi nzuri zilizofanywa na wafanyakazi wote wakiwa wenye shauku. Kijana mmoja alisema:

> "Kabla ya mradi wa READY+ nilijisikia mpweke, sikuwa na rafiki yeyote na sikupenda kwenda shule kwa sababu nilihisi kubaguliwa. Kwa sasa baada ya kupata msaada kutoka kwa wahudumu wa afya na shangazi Leo, nasikia kujiamini. Nina marafiki. Mama yangu ana furaha zaidi na yeye na baba yangu wa kambo ni wafuasi wazuri zaidi wa matibabu yao kama ambavyo hata mimi nafanya.

Ninawapongeza wafanyakazi wote wa shirika la Frontline AIDS kwa kujitolea kwao na kwa kazi nzuri ya kustaajabisha. Kwa kuwa huu ni mwezi wangu wa mwisho kwenye nafasi yangu hii ya kazi, nawatakia Maisha mema katika miaka ijayo.

# Kongamano la PATA 2023

NA, ANGELITA SILVA, MENEJA WA MASOKO NA MAWASILIANO NA HELEEN SOETERS, MENEJA MWANDAMIZI , MRADI WA AFRIKA WA TIBA YA WATOTO NA VIJANA WAKUBWA (PATA)

**Kongamano la mwaka 2023** likiwa na mada isemayo: Uso wa Huduma: Watoa huduma za afya na Jamii kwenye Mstari wa Mbele wa Utoaji wa Huduma ya Watoto na Vijana wakubwa wanaoishi na VVU katika bara la Afrika, ulitumia mbinu ya kushirikiana na kujifunza ili kukuza mashirikiano ya kikanda, kujenga uwezo na ushirikiano wa makundi rika kwenye mitandao yote ambapo mradi huu unatekelezwa na hata nje ya eneo la mradi. Tukio hili mseto lilijumuisha ushiriki kwa njia ya mtandao na mahudhurio ya washiriki ya moja kwa moja ; yaliwahusisha watoa huduma wa afya, wasaidizi wa makundi rika na makundi mengine pia; na yalitilia mkazo sauti za wale waliokuwa mstari wa mbele.

**Mada tatu zilikuwa za msingi zaidi wakati wa Kongamano:**

1. Kukuza uthabiti na ustawi wa watoa huduma za afya: kuwajali wale wanaotujali sisi.
2. Kutoa fursa kwenye warsha za mafunzo zinazochochea Mawazo kwenye majadiliano ndani ya nchi, kubadilishana uzoefu na kubuni majibu ya matatizo yanayopatikana ndani ya nchi.
3. Kukuza safu ya wataalamu walio mstari wa mbele ili waweze kukabiliana na changamoto za utoaji wa huduma za kupambana na maambukizi ya VVU.



Kwenye satelaiti saba zinazomulika nchi tano ambapo miradi ya READY+ inaendelea, Kongamano PATA liliwasaidia washiriki zaidi ya 220, pamoja na watoa huduma za afya 137, ili kuhudhuria kongamano wao wenyewe. Zaidi ya hapo, kwenye satelaiti 22 zilizopo kwenye nchi 13, wasaidizi wa rika 150 walihudhuria kongamano, ikionesha jukumu muhimu sana la sauti za vijana katika kuchagiza mwelekeo wa huduma za afya za baadaye. Ntombikayise Ncube, ambaye ni mkufunzi wa rika anayehudumu kwenye asasi ya Zimbabwe Young Positives alisema: "Watoa huduma za afya wanapaswa kujenga mahusiano rafiki zaidi, wawe wanaofikika na wawe tayari kutoa misaada kila wakati vijana rika wanapokuwa na shida."

Tunapaswa pia kuendelea kuwafunza vijana wadogo ili wawe mawakala wa mabadiliko" Kama sehemu ya mkakati wa kimataifa wa kutokomeza UKIMWI miongoni mwa vijana wadogo na wakubwa ifikapo mwaka 2030,Kongamano hili lilionesha mshikamano mkubwa na jitihada katika kufikia lengo la kuutokomeza UKIMWI. Kongamano lilikazia majadiliano ya matibabu ya UKIMWI kwa Watoto na vijana wakubwa.

Linaendelea kusimama kama mwanga wa miaka ijayo ambapo watoa huduma za afya na watetezi wa vijana wanaungana kwenye maamuzi yao ili kuandaa dunia ambapo madhara ya maambukizi ya VVU hayatakuwepo kwenye kijazi kijacho.

## FUATILIA HARAKATI! Kalenda ya Matukio

| | |
|---|---|
| 1 Machi | Siku ya Kutokomezwa kwa Ubaguzi |
| 2 Machi | Siku ya Maamuzi ya Mwanamke |
| 8 Machi | Siku ya Kimataifa ya Wanawake |
| 11–22 Machi | Kamisheni Juu ya hali za wanawake |
| 11 Aprili | Siku ya Kimataifa ya Haki na Afya ya Uzazi |
| 29 Aprili–3 Mei | Kamisheni juu ya Idadi ya watu na maendeleo, ikitathmini miaka 30 ya utekelezaji wa malengo ya Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya watu na Maendeleo |
| 19-25 Mei | Wiki ya Chuo cha READY, Eswatini |

Unga mkono harakati za READY kwa kufuatilia matukio na machapisho haya:

Facebook: READYMovement | Twitter: @READY_Movement | Instagram: @readymovement

Kwa kutumia #WeAreREADY. Na kutembelea mtandao https://frontlineaids.org/ready na https://www.yplusglobal.org/projects-ready-2.0 kwa habari na masasisho.

**Shukurani!**
Y+ Global na Frontline AIDS wanapenda kutoa shukrani kwa:

- Vijana wote walio mstari wa mbele kwenye kazi hii.
- Washirika wote wanaotekeleza miradi ya READY: Ajuda de Desenvolvimento de Povo para Povo (ADPP), Mkutano wa Uratibu wa asasi zisizo za kiserikali (CANGO), Mradi wa Afrika wa Matibabu ya Watoto na vijana wakubwa (PATA), Regional Psychosocial Support Initiative( REPSSI), Young Africa and Zvandiri
- Mashirika mengine yote ambayo ni sehemu ya harakati za READY
- Wizara ya mambo ya Nje ya Uholanzi na Mfuko wa Wakfu wa Elton John wa kupambana na janga la UKIMWI, kwa misaada yao.